

Ukweli Hauna Kutu Pambazuko

Toleo Namba 012

Jumatatu Septemba 26- Oktoba 2, 2022

Uk. 4: Mwigulu anapata wapi jeuri?



**Wabunge
Kenya
watamani
ulafi
Uk. 7**

**‘Mauzauza’
ya uchumi
wa kidijitali**

Kifo kuwa hiari kufikia mwaka 2045 - Uk. 16

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Rais unda Kurugenzi Huru ya Kuchunguza Polisi

SIFA za Jeshi la Polisi Tanzania zimekuwa zikibadilikabadilika kila mara kutegemea nani ni mkuu wa nchi na zaidi sana nani ni Inspekta Jenerali (IGP) kwa wakati huo.

Hakuna siri hata kidogo kwamba kila IGP anakuwa na zama zake; wapo waliofanya kazi vizuri - bila kujiingiza kwenye mtungo wa majambazi, wauza dawa za kulevywa, majangili na hata wanyang'anyi wengine, wakiwamo mafisadi.

Lakini pia wapo wakuu wa jeshi letu la Polisi walioamua kujiunga na magenge ya hovywa kwa ajili ya kupata utajiri haramu wa harakaharaka.

Hawa wakuu wa kundi la pili ndio walioharibu kabisa nidhamu na sifa ya jeshi hilo lenye majukumu makubwa ya kulinda watu na mali zao. Hawa walishiriki kutesa, kubambika kesi na kuamuru wasaidizi wao kupora mali halali za wananchi ilimradi wao wapate kikubwa na neema kwa kuumiza wengine.

Ni hawa wa kundi la pili ndiyo walikuwa wakijiona mungu-watu, kiasi kwamba hawakuwa hata na chembe ya kumuogopa Amiri Jeshi Mkuu kwa sababu ambazo wanazijua wao wenyewe.

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa na habari nyingi katika vyombo vya habari na hata mitandao ya kijamii inayoeleza maovu yanayoelekezwa kwa jeshi hilo; kwamba watuhumiwa wamepokwa mali zao, kuibwa kwa vielelezo - hasa fedha na dawa za kulevywa, kuteswa na hata baadhi ya watuhumiwa kufia mikononi mwa watendaji wa jeshi hilo.

Kunapotokea matukio haya ya hovywa, ni watendaji wa jeshi hilihilo ndiyo hupangwa kuchunguza kilichotokea, hatua ambayo, kwa mizania yoyote ile haiwezi kuwa ya haki hata kidogo.

Hivi inawezekanaje mtuhumiwa akachunguzwa na watuhumiwa wenzake? Kwamba linalotuhumiwa ni jeshi, na wachunguzi wanakuwa wao. Hapa hakuna haki inayoweza kutendeka, isipokuwa ni kufichwa kwa ukweli na watuhumiwa kuachwa huru, hata kama kuna kila dalili kwamba walitenda uovu.

Ni kutokana na sababu hizo na kuongezeka kwa tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, sisi katika Pambazuko tunaona wakati umefika sasa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuunda Kurugunzi Huru ya Upelelezi kwa Polisi.

Tunapendekeza kwamba ikiwa Rais ataridhia kuundwa kwa kurugenzi hiyo, iwe ni sehemu ya watendaji walioko ofisini kwake - Ikulu ili kuwepo na ufanisi na kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa kila uchunguzi unaofanywa dhidi ya Polisi na watendaji wake.

Ni kurugenzi hiyo, ambayo itaundwa na watu weledi, wazalendo na wafia nchi ambao umma hautakuwa na chembe ya shaka juu ya tabia zao ndani ya utendaji wa kurugenzi hiyo maalum.

Dhamira kuu ya kurugenzi hiyo ni kuwa chombo chenye ufanisi, huru na kisichoegemea upande wowote katika uchunguzi na usimamizi ambacho kinatenda haki na kwa maslahi ya umma, huku kikidumisha viwango vya juu vya uadilifu na ubora.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Mkijua misingi ya demokrasia, hamuwezi kamwe kutengeneza mikakati ya kisiasa kuiua demokrasia yenyewe – Godbless Lema- aliwahi kuwa Mbunge wa Arusha Mjini kupitia Chadema.

Mwigulu anapata wapi jeuri?

Na Asha MABROUK

KIMSINGI viongozi wote wa umma – kuanzia mwajiriwa nambari moja; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni watumishi wa wananchi.

Wananchi ndiyo wanaawalipa mishahara yao na stahiki zingine. Ujira wao, unatokana na kodi za wananchi, bila kujali nani analipa kiasi gani cha fedha kwenye Hazina ya Taifa.

Hata hivyo, kwa wanasiasa wengi wa Tanzania, kung'amua kwamba waajiri wao, wanapopata dhamana serikalini ni wananchi, huja wakati wa uchaguzi tu,

Ni katika kipindi hicho, wanasiasa wanaoomba kuchaguliwa ili waingie bungeni na baadaye kupata dhamana za uwaziri au nafasi zingine serikalini, huonekana “wakiabudu” wapigakura wao.

Ni kwenye kipindi hicho huonekana wakiwa karibu zaidi na wananchi, huku wengine wakipiga goti au kumwaga chozi wakililia kura za hao waajiri wao.

Lakini, isiyokuwa bahati, wakishapata ushindi na wengine kumegewa nafasi za uwaziri, basi huwageuka walipa mishahara wao na kuwaona “siyo kitu.” Hawana muda tena hata kuzungumza nao.

Kibaya zaidi wanapokuwa na dhamana kubwa zaidi, hujenga kiburi na kupandisha mabega, huku wakijimwambafai kwamba wao ni werevu zaidi na wajuvi wa mambo mengi, hata kama wana uelewa mdogo.

Siyo mara moja wala mbili, Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, ameonekana na kusikika akivaa dalili za viongozi wenye jeuri kwa waaajiri wao.

Uzuri wa Dkt. Mwigulu ni usikivu, kwamba hufuatilia malalamiko na kero za wanaomlipa ujira wake, lakini hukwama kwenye kutoa ufafanuzi wa jambo au kero zinazozungumzwa, hata kuwa na kauli zenye ukakasi.

Ni Mwigulu huyu aliwahi kuwaeleza



Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango

walipa ujira wake kwamba “kama hawapendi jambo fulani, basi wahamie Burundi.” Kauli za namna hii siyo nzuri hata kidogo. Hazina ustaarabu na hazimpendezi mtu wa haiba na usomi wake.

Dkt. Mwigulu pia amekuwa akifanya shingo yake ngumu kuhusu malalamiko ya kuwepo tozo. Alishindwa kusikiliza wananchi hadi aliposhinikizwa na Kamati Kuu ya chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hakuonekana kuchukua hatua kufuta chozi wananchi kuhusu tozo lukuki kwenye fedha zao.

Ni wakati muafaka sasa kwa wanasiasa wenye dhamana kusikiliza kero za wananchi na kujijali kwa kuzitolea ufafanuzi na pengine ufumbuzi, badala ya kusubiri viongozi ama vikao vya juu zaidi kuingialia kati na kushinikiza ndipo hatua zichukuliwe.

Watanzania wasahaulifu au hawajali?

Na Dkt. Bullet RUHINDA

WATANZANIA tu watu wapole na wanaoamini kila tunachoambiwa na walio madarakani. Nachelea kusema kwamba wananchi wengi hawana muda wa kuchambua mengi yatolewayo na watawala.

Sijui inasababishwa na nini kati ya hulka na elimu, kwa maana kwamba ni hulka ya wengi kutohoji au elimu yetu hainoi bongo zetu ili watu waweze kuhoji kila wanachoambiwa na “wakubwa.” Nitatoa mifano michache kuthibitisha hilo.

Siyo muda mrefu sana uliopita suala la Katiba tuliambiwa halina nafasi kwa sababu huu ni muda wa maendeleo.

Tukaambiwa kwamba wananchi wanahitaji maji, barabara, huduma za afya na elimu na nyingine kama hizo. Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema Katiba haiteti chakula mezani, wengine wakasema mchakato wa Katiba ni ghali sana, pesa ambazo zingetumika kwa mchakato huo zielekezwe kwenye shughuli za kimaendeleo.

Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuonesha umuhimu wa Katiba mpya, hoja zote za kutaka maendeleo kwanza zimezimika.

Kinachoshangaza ni wananchi wengi kutohoji kwamba kama Katiba sasa inazungumzika, je, tayari tumepata barabara, maji elimu na yote waliosema yapatikane kwanza? Je, sasa Katiba italeti chakula mezani? Kwa nini wananchi hatuhoji mkanganyiko huu? Ni kwamba tumeridhidhika au hatujali?

Mfano wa pili ni trilioni za shilingi ambazo tuliaminisha kwenye awamu ya tano na aliyekuwa rais wetu, John Magufuli (sasa marehemu) kwamba nchi itazipata kutokana na madini.

Aliyekuwa ‘kipenzi’ cha Rais Magufuli, profesa wa sheria, Palamagamba Kabudi aliliambia taifa kwamba nchi inapata asilimia 50 kwa hamsini kati serikali na



John Magufuli

kampuni za madini.

Tulisahau kumuuliza kama sisi hisa zetu ni asilimia 16, tutawezaje kupata 50/50 na kampuni zinazomiliki asilimia 84? Je, akili ya Watanzania ilishindwa kuliona hilo?

Tuliambiwa trilioni za fedha nchi inazopata zinaweza kumnunulia kila Mtanzania angalau gari aina ya Noah! Wote tulishangilia kwa ‘ushujaa’ wa akina Profesa Kabudi kwa kuongoza majadiliano na ‘mapambano’ dhidi ya kile utawala uliopita ulikuwa ukiimba kuwa ni unyonyaji wa kampuni za madini.

Ni majuzi tu Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, aliuiliza mbona hizo kesi zitakazotupatia kiasi kikubwa cha fedha; kwa trilioni nyingi, hazitolewi hukumu? (swali ambalo lilitukumbusha kwamba tuliahidiwa ‘matrilioni’).

Majibu aliyoaambia kutoka kwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango ni kigugumizi na maneno yasiyoeleweka kwa wengi (hata kwa mheshimiwa spika) ya TRAB na TRAT!

Akamalizia kwamba “tayari tunapata gawio kama kawaida.” Watanzania kama kawaida yao ya kutopenda kuuliza au kwa kutojali, wameshindwa kuhoji, je, trilioni za shilingi tulizoahidiwa, ziko wapi?

Je, Watanzania, ni kipi kisichokweli tutakachoambiwa kitushtue na kuanza kuhoji? Je, tutaendelea kuridhika mpaka lini?

Serikali sasa yakabili Ebola

Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania imechukua shadhari zote za kukabili mlipuko wa ugonjwa wa ebola ambao unaripotiwa kuua watu sita nchini Uganda.

Tayari wataalamu wa afya wamejipanga maeneo ya mipakani, viwanja vya ndege na hata bandari kudhibiti kuingia kwa ugonjwa.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Aifelo Sichwale amesema “tumejipanga kuhakiisha nchi na watu wake wanakuwa salama dhibi ya ugonjwa huo.”

Dkt. Sichwale amebainisha pia kwamba serikali, kupitia wizara ya afya, imeandaa timu za dharura endapo kutaripotiwa kuwepo kwa dalili za ugonjwa huo eneo lolote ndani ya Tanzania.

Mikoa ambayo imeanza kufuatiliwa kwa ukaribu zaidi ni pamoja na Arusha, Dar es Salaam, Geita, Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma na Kilimanjaro.

Tayari Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel ameliambia taifa kwamba “Tanzania hakuna taarifa zozote za kuwepo kwa ugonjwa huo.”



Dk. Mollel

Polisi watuhumiwa kumvua nguo binti mbele ya baba

Na Mwandishi WETU

JESHI la Polisi Tanzania linatuhumiwa kwa kutenda ukatili kwa kumlazimisha msichana wilayani Serengeti, mkoani Mara, kuvua nguo mbele ya baba yake mzazi.

Msichana huyo, Tabitha Mwise (22), alinukuriwa na gazeti la Mwananchi akieleza kwamba baba yake ambaye ni miongoni mwa watuhumiwa waliokamatwa na jeshi hilo, Mwise Simon (54), akiwa nyumbani kwake

Septemba 21, mwaka huu, polisi walimlazimisha kuvua nguo na kumshinikiza kueleza silaha waliyodai baba yake anaimiliki.

Tayari Jeshi hilo limekiri kuua watu watatu – kwa kuwapiga risasi, wilayani humo kwa maelezo kwamba ni watuhumiwa wa ujambazi. Mwise ni miongoni mwa waliouawa.

Thabisa anaeleza kwamba aliwaeleza kwamba hakuwahi kumuona baba yake akiwa na silaha, lakini polisi waliendelea kumshinikiza, huku akipewa kipigo, kueleza anakoficha silaha mzazi mwake huyo.

“Kwanza walifika kwa kishindo alfajiri ya Septemba 21, mwaka huu wakiwa na magari mawili; wakavunja milango na kuwatoa nje wote waliokuwemo ndani huku wakimtembezea kipigo kila aliyekuwa mbele yao,” amesema binti huyo

Amesema mlango wake ulipovunjwa na yeye kutolewa nje kwa vipigo, alimkuta baba yake na ndugu wengine wakiwa tayari wametolewa nje huku wakipigwa kulazimishwa kuonyesa silaha zilipofichwa.

“Baada ya kuwajibu kwamba sifahamu bunduki ilipo na wala sijawahi kumwona baba yangu akiwa na bunduki, askari wale waliendelea kunishambulia sehemu mbalimbali za mwili huku watuamuru mimi na baba kuvua nguo zote,” amesema

Wabunge Kenya watamani ulafi

Na Mwandishi WETU, Nairobi

NAIBU Rais wa Kenya Rigathi Gachagua wakati akitoa shukrani baada ya kuapishwa kwa nafasi aliyonayo – Septemba 13, mwaka huu jijini Nairobi, ‘aliuponda’ uongozi uliopita kwa kuacha Hazina bila fedha.

Kwamba serikali iliyoongozwa na Rais Uhuru Kenyatta, ilikuwa ikitumia fedha vibaya kiasi cha kuacha fedha kiduchu, huku akieleza “ugumu ulioko mbele kuendesha serikali kwa kukosa fedha.”

Kauli hiyo ya Gachagua inabeba maneno ya Rais William Ruto na serikali anayoongoza iliyoingia madarakani baada ya kutangazwa washindi katika uchaguzi mkuu uliofanyika Agosti 9, 2022.

Hata hivyo, kauli hiyo inaweza kuwa tofauti na matazamiaji wa wabunge wengi wa chama cha viongozi hao wakuu – Kenya Kwanza, ambao tayari wameanza kutaka kuongezwa marupurupu.

Hata kabla ya kuanza kuwatumikia wananchi waliowachagua, wabunge hao, wengi wakitoka chama cha Ruto, wanadai ni wakati mzuri kwao kuandaliwa posho zaidi ili waweze “kuwatumikia vyema” wananchi.

Wabunge hawa wanasahau kuwa wanadai posho na nyongeza ya marupurupu wakati wananchi wanaocheleza kuwapigania – wengi wakikabiliwa kwa njaa na maisha magumu baada ya kupanda kwa bei ya unga, mafuta na gharama zingine.

Jumatatu iliyopita, Septemba 19, wabunge hao, wakiwa katika mkutano wao elekezi juu ya namna ya kutekeleza majukumu yao, waligoma kuhutubiwa na Mwenyekiti wa Tume ya Mishahara (SRC), Lyn Mengich wakitaka aje na jibu zuri la namna ya kuongeza malipo yao na siyo “hotuba tu.”

Wakiongozwa na Spika wa Bunge la Kitaifa, Moses Wetang’ula, wabunge hao 349 walimtaka Mengich ahakikishe anarudisha marupurupu yao, ikiwamo



Spika Watengula

posho ya kikao, safari na kile walichocheza kuwa stahiki zingine.

Hata hivyo, Spika Watengula aliwahakikishia wanasiasa hao waliochaguliwa na wananchi (wengi walipa kodi masikini) kwamba watapata wanachostahili.

Silvanus Osoro, Mbunge wa Mugirango Kusini alisikika akisema kuwa wabunge wanakabiliwa na majukumu makubwa, mengi yakiwa kusaidia wananchi, hivyo ni vyema wakapata fedha zaidi ili msaada uwe wa uhakika na mkubwa.

“Siyo busara pia kuendelea kuondoa marupurupu yetu, lazima yawepo. Hayafai kuondolewa wakati gharama za maisha zimepanda,” aliongeza mbunge huyo akizungumza na waandishi wa habari nje ya ukumbi wa mikutano.

SRC ilifuta marupurupu ya Sh5,000 kwa kila kikao, ambazo wabunge 349 na maseneta 67 walikuwa wakilipwa kwa kuhudhuria vikao vya bunge.

Hii ina maana kuwa kila mbunge atakosa Sh80,000 kila mwezi kwa kuhudhuria vikao, hata bila kutoa mchango wowote. Hii ni kando na mishahara yao ya kawaida ya Sh710,000 pamoja na marupurupu mengine.

Ni nani anayemiliki taifa?

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

MAMBO tunayoyaona sasa hapa Tanzania, mathalan kuhusiana na kelele juu ya 'tozo' za miamala ya fedha ni mfano mzuri sana juu ya hoja ya umiliki wa taifa.

Mamlaka imekaa mikononi mwa nani? Nani anafanya uamuzi juu ya maisha ya watu? Nani anammilikisha mwingine madaraka? Nani anao uwezo wa kumuondoa mwingine madarakani?

Hapa ni suala zima la uwajibikaji na uwajibishaji. Kwa upande mwingine nani anayemiliki ardhi na raslimali za taifa? Nani anayetunga sheria za kuongoza na kuratibisha uendeshaji wa nchi?


Je, sheria hizo zinatungwa kwa kulinda maslahi ya nani? Ni chombo gani kina dhamana ya kusimamia tafsiri na utekelezwaji wa sheria hizo? Nani anayeteua watendaji wakuu katika mhimili unaosimamia sheria?

Majibu ya maswali kama hayo ndio huonyesha ni nani anayemiliki taifa. Mambo kama hayo lazima yatiliwe maanani katika uandishi wa katiba na sheria, kwani ndio huratibisha uwiano wa matarajio ya watu.

Ikiwa watawala ndio wanaomiliki nchi, basi katiba na sheria zitatumwa kwa namna ya kulinda nafasi za watawala hao na maslahi yao. Hapo ndipo tunasema kuwa taifa lina serikali iliyopita kiasi (maximum government).

Hali kama hiyo huminya uhuru na ushiriki wa raia katika uendeshaji wa nchi. Tena hali kama hiyo huishia kubebesha mizigo ya kodi kwa raia ili kutunza serikali na mahitaji yake. Suala zima la mvutano kati ya serikali iliyopitiliza kiasi na serikali kidogo (minimum government) vinazungukia katika mambo kama hayo.

Hapa ndipo tunaingia katika upimaji wa dhana mbili muhimu katika kujua umiliki wa taifa. Dhana hizo ni



Ramani ya Tanzania

demokrasia na uwajibikaji.

Tukumbuke kwamba katika kuzungumzia kipengele cha 'watu' nilishughulikia kwa kiasi suala la uwajibikaji. Uwajibikaji ni dhana muhimu katika maadili ya siasa na utumishi.

Ikiwa taifa lina watu waliotengenezwa vizuri ni wazi kwamba watu hao watatengeneza jamii ya watu waadilifu wanaowajibika ipasavyo kwa jamii.

Tulizungumza pia kwamba jamii ndio muundo wa msingi katika kuundwa kwa taifa. Kwa hiyo, taifa lenye jamii ya watu wazuri wanaowajibika, ni taifa la watu wanaowajibika kwa jamii.

Katika uwelewa huo ndipo nafasi wapewazo watu, ikiwa ni katika utawala au kitaaluma, wote huzipokea kama dhamana na kama nafasi ya kutumikia jamii na kamwe siyo haki ya awaye yeyote. Uelewa huu ndio hugeuka kuwa maadili ya jamii.

Dhana nzima ya uwajibikaji ikaopo vizuri ndipo hata utengenezaji wa miundo ya kidemokrasia huwa rahisi. Iwapo vyeo walivyonyavyo watu siyo haki zao, bali ni utumishi na wanatumika kwa kuwajibika kwa jamii.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mkazo uwekwe kwenye afya ya akili

NILIANZA safari ya uandishi wa makala zaidi ya miaka 20 iliyopita. Kwa hakika ni miaka 25, kwani makala yangu ya kwanza kabisa ilichapishwa gazetini mwaka 1997.

Wazo la uandishi wa makala lililokana na ushauri wa mwanahabari mmoja mkongwe wa habari za michezo ambaye alikuwa mwanachuo mwenzangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mlimani).

Mwanahabari huyo alinielea kuwa alidhani ningeweza kuwa mwandishi bora endapo ningeingia kwenye fani hiyo. Wiki chache baadaye, makala yangu ya kwanza kabisa ilichapishwa kwenye gazeti la kila wiki (enzi hizo) la “Sanifu.”


Gazeti hilo ndio la kwanza nchini Tanzania kuandika habari za udaku. Naam, nilianza uandishi wa makala magazetini kama “mwanahabari wa udaku.” Baadaye nikapata fursa kwenye magazeti mengine mawili ya udaku – Komesha na Kasheshe.

Baada ya muda nikaanza uandishi wa makala kuhusu masuala ya siasa. Hata hivyo, makala hizo zilikuja kunigharimu mbeleni, lakini nafasi haitoshi kueleza kuhusu hilo kwa sasa.

Miaka kadhaa baadaye, katika kukabiliana na changamoto zilizotokana na uandishi wa makala hizo za siasa, nilikutana na maandiko kuhusu kitu ambacho nimekipa jina “jinsi ya kuwa mtu bora” ikiwa ni tafsiri ya “personal development” kwa Kiingereza.

Nikaanza kuchapisha makala kuhusu mbinu mbalimbali za kumfanya mtu awe bora, au aweze kuboresha ubora wake. Tofauti na makala za siasa ambazo zilinitengezea maadui, hizo za “mtu bora” siyo tu zilinitengezea marafiki wengi, bali pia zimekuwa msaada kwa watu mbalimbali.

Hadi muda huu nimeshachapisha vitabu viwili -Jinsi ya Kuwa Mtu Bora



-toleo la kwanza na la pili.

Lengo la makala hii siyo kueleza historia yangu katika uandishi wa makala au kunadi vitabu vya “mtu bora”. Nimesukumwa na taarifa mbalimbali huko Tanzania kuhusu matukio yanayodhaniwa kuwa yanachangiwa na matatizo ya afya ya akili (mental health problems).

Kwa bahati mbaya, matatizo ya afya ya akili siyo tu yanaonekana kama suala geni, bali pia kuna hisia kuwa siyo matatizo ya kiafya.

Kwa bahati nzuri, licha ya uwepo wa tiba za kitabibu, kuna njia mbalimbali zilizo ndani ya uwezo wetu zinazoweza kuzuia, kupunguza na hata kumaliza matatizo hayo. Miongoni mwa mbinu hizo ni tahajudi (meditation), moja ya aina za “mindfulness” (tuite “kujitambua”).

Itaendelea...

Tanbihi: Katika toleo lililopita, tarehe ya kufariki dunia kwa Malkia wa Uingereza Elizabeth II ilikosewa. Usahihi ni kwamba aliaga dunia Septemba 8, 2022.

‘Mauzauza’ ya uchumi wa kidijitali

Na Waandishi WETU

NDOTO ya Tanzania kuvuna mapato makubwa kupitia uchumi wa kidijitali, huenda ikachukua muda mrefu zaidi kwa sababu ya kuingizwa siasa katika utekelezaji wake.


Kwamba serikali imekuwa “ikipiga kelele” kuhusu kuwepo kwa mapato makubwa kutokana na uchumi wa kidijitali, lakini hata bajeti iliyotengwa; 2022/2023 - kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kuingia kwenye mfumo huo wa uchumi ni kiduchu mno.

Hadi sasa Tanzania ina vituo vitano tu vya kupokea na kusukuma data ambavyo viko mikoa mitano; TIX cha Dar es Salaam, AIXP cha Arusha, DIXP cha Dodoma, MIXP cha Mwanza, na ZIXP cha Zanzibar, wakati angalau hadi sasa Tanzania ingepaswa kuwa na kituo kimoja kila mkoa. Tanzania ina mikoa 30.

Pambazuko limebaini kuwa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo ni Sh. 282,056,786,000 haielezi kinagaubaga fedha inayotengwa kwa ajili ya kuongeza vituo hivyo ili kwenda sambamba na kauli za serikali kushadadia uchumi wa kidijitali ambao msingi wake umo ndani ya mawasiliano ya nguvu na uhakika ya uimara wa intaneti, hasa data.

Gazeti hili limebaini kwamba hadi Juni 2021, ni asilimia tano pekee ya miamala ya data ndiyo inayokusumwa na kupokelewa na vituo hivyo, huku asilimia 95 ikiwa inasukumwa na vituo vya data vilivyoko nchi jirani za Rwanda, Uganda na Kenya.

Vituo vya kupokea na kusukuma data, yaani “internet exchange points (IXPs),” hufanya kazi kama ambavyo minara ya kupokea na kusukuma mawimbi ya maongezi ya simu, yaani “signal relay



Mtawanyiko wa Vituo vya Kupokea na Kusukuma Data nchini Tanzania. Picha imechukuliwa kutoka kwenye tovuti ya TCRA

‘Mauzauza’ ya uchumi wa kidijitali

Inatoka Uk. 10

stations,” hufanya kazi zake.

Vituo hivi ni vitovu vya kuwaunganisha wateja wa intaneti na watoaji wa huduma za intaneti nchini. Watoa huduma hawa ni pamoja na TTCL, Vodacom, Tigo, Halotel, Zantel, Simbanet, Raha, Benson, na wengine wengi.

Data inayoanzia ndani ya Tanzania na hatimaye kutua ndani ya nchi hiyo, mapato hubaki nchini, hata hivyo, kutokana na kiasi kikubwa cha data “barabara” zilizoko nje ya Tanzania, sehemu kubwa ya mapato hayo huenda kwenye nchi zenye vituo vya data vya Uganda, au Rwanda, au Kenya. Tanzania, hulazimika kulipia ushuru wa kutumia “barabara za data” zisizokuwa zake, yaani “traffic capacity charge.”

Sababu ya msafara wa data kuanzia Tanzania, kusafiri kwa kupitia kwenye “barabara za data” zilizoko nje ya Tanzania, na hatimaye kutua tena Tanzania, ni ufinyu wa “barabara za data” zilizoko ndani ya Tanzania. Ufinyu huo ama ni kwa sababu ya kuharibika kwa baadhi ya vituo vya kupokea na kusukuma data, nguvu ndogo ya vituo hivyo, au ni kwa sababu ya uchache wa vituo hivyo.

Utata wa takwimu za TCRA kuhusu data

Pambazuko limebaini kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nayo haina kumbukumbu sahihi za kiasi gani cha fedha zinakusanywa kutokana na kupokea ama kusukuma data kwa kuwa taarifa rasmi za mamlaka hiyo hazielezi uzito wa data, bali inataja tu idadi ya kadi za simu zilizosajiliwa.

Uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwa kati ya Aprili na Juni 2022, hakuna takwimu zinazoonyeshwa na TCRA kuwa ni kiasi gani cha ujazo wa data zinazosafirishwa na kupokewa na

watumiaji walioko nchini.

Hata hii inatia shaka endapo mapato yanayotajwa ndiyo halisi yanayotakiwa kuingia kwenye Hazina ya Taifa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Hata hivyo, taarifa zilizoonwa na Pambazuko ni zile za mawasiliano ya maongezi yaliyofanyika ndani ya mipaka ya Tanzania – kwa kipindi cha miezi hiyo miwili, kuwa ni jumla ya dakika 29,439,206,770. Mawasiliano ya maongezi yaliyofanyika kati ya Tanzania na nchi za nje ni jumla ya dakika 21,170,601.

Meseji zilizotumwa ndani ya mipaka ya Tanzania ni 37,107,937,725. Meseji zilizotumwa kati ya Tanzania na nchi za nje ni 872,785,354. Na idadi ya kadi za simu zilizotuma au kupokea data ndani na nje ya Tanzania ni 29,169,958.

Kwa mujibu wa bei zilizotajwa na TCRA katika taarifa yake ya Juni, 2022, bei ya maongezi kwa simu za ndani ya nchi ni wastani wa Sh. 32 kwa kila dakika; bei ya maongezi kwa simu za kimataifa ni wastani wa Sh. 1,520 kwa kila dakika; bei ya meseji za ndani ya nchi ni wastani wa Sh. 11 kwa kila meseji, wakati bei ya meseji za nje ya nchi ni wastani wa Sh. 202 kwa kila meseji. Na bei ya data kwa mawasiliano ya ndani ya nchi ni wastani wa Sh. 8 kwa kila megabaiti moja.

Hivyo, kati ya Aprili na Juni mwaka huu, maongezi kwa simu za ndani ya nchi yalikuwa na thamani ya Sh. 942,054,616,640; maongezi kwa simu za nje ya nchi yalikuwa na thamani ya Sh. 32,179,313,520; meseji za ndani ya nchi zilikuwa na thamani ya Sh. 408,187,314,975; meseji za nje ya nchi zilikuwa na thamani ya Sh. 176,302,641,508; na thamani ya kifedha ya data haiwezi kufahamika kwa kuwa ujazo wake haukutajwa popote; siyo

‘Mauzauza’ ya uchumi wa kidijitali

Inatoka Uk. 11

TCRA wala idara nyingine, ikiwamo taarifa za Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA).

Naibu Spika angwiwa hofu

Ni kutokana na hofu ya kufikia malengo na matamano ya Tanzania kupata maendeleo zaidi kupitia uchumi wa kidijitali, 21 Septemba 2022, akiwa Jijini Dodoma wakati wa kikao cha Bunge, Naibu Spika wa Bunge, Idd Azan Zungu, ameitaka serikali kuongeza nguvu na kuangalia namna nzuri ya kuifanya ndoto kuwa hali halisi.

Zungu alisema kwamba, kasi ndogo ya ujenzi wa miundombinu ya tehamu kwa ajili ya kupokea na kusukuma data, inalifanya taifa kuchelewa kukamilisha mradi wa kujenga taifa la kidijitali.

Mtaalamu wa Tehama nchini Tanzania, Joseph Kimbe ameliambia Pambazuko kwamba serikali inaweza kupata mapato makubwa zaidi kupitia kwenye miamala ya data kuliko kodi inayopatikana kutoka kwenye miamala ya simu za maongezi.

Kimbe anaeleza wasiwasi wake kuhusu kasi ya serikali na tambo za kuingia uchumi wa kidijitali wakati hali halisi haionyeshi dhamira ya vitendo ya kupata mapato makubwa zaidi kupitia matumizi makubwa ya data; kuingia na kutoka ndani ya Tanzania.

Kupitia hotuba ya bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Waziri Nape Nnauye alilitangazia taifa kwamba, serikali inatekeleza “mapinduzi ya kidijitali” ambayo yataweka msingi wa kulipeleka taifa kwenye “Uchumi wa Kidijitali.” Hata hivyo, hotuba hiyo haina mengi ya kuonyesha nia hiyo ya serikali.

Mwandishi Dan Tapscott wa Marekani kupitia kitabu chake, “The Digital Economy: Rethinking Promise and Peril in the Age of Networked Intelligence (1995).” Anaeleza kuwa uchumi wa

kidijitali ni mfumo wa wanunuzi na wauzaji wa bidhaa na huduma kubadilishana ujazo mkubwa wa taarifa kwa njia ya mitandao ya kompyuta, kwa kasi na ufanisi mkubwa bila ulazima wa kukutana uso kwa uso.

Pia wataalamu wa Tehama wa Tanzania wanaeleza kuwa mradi wa kujenga taifa la kidijitali unahusisha majukumu makubwa matatu; uchumi wa kidijitali, jamii ya kidijitali, na dola ya kidijitali.

Waziri Nape anasema kwamba serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan tayari imechukua hatua kadhaa za kuhakikisha uchumi wa kidijitali unafikiwa na Watanzania kufaidi matunda yake.

Hata hivyo ni pamoja na kukamilisha uandaaji wa mkakati wa taifa wa intaneti yenye kasi; kukamilisha uandaaji wa rasimu ya mkakati wa uchumi wa kidijitali; na kukamilisha uandaaji wa mwongozo wa mageuzi ya kidijitali.

Hata hivyo, Pambazuko halikuziona nyaraka hizi mahali popote mtandaoni, ingawa mmoja wa wasaidizi wa Waziri Nape amesema uandaaji wa mikakati hiyo iko katika hatua nzuri na baadaye itawekwa kwa umma. Hakutaka kutajwa jina lake gazetini.

Sera ya Taifa ya Tehama ya Mwaka 2016 inasema kwamba, Tanzania inakusudia “kuwa na miundombinu ya tehamu inayoaminika, inayosikilizana, na endelevu kwa ajili ya kufanikisha mtandao wa kidijitali unaofanya kazi muda wote.”

Vilevile Pambazuko limeuona Mpango Mkakati wa “Wizara ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano” unaotekezwa kuanzia 2021 hadi 2025 bila kutaja viashiria vya ufanisi kuhusiana na ujenzi wa uchumi wa kidijitali, serikali ya kidijitali, mahakama ya kidijitali wala ujenzi wa Bunge la kidijitali.

Maana ya dola ya kidijitali



Na Mwandishi WETU

SIYO jambo geni kusema kwamba sasa Tanzania iko katika “Mapinduzi ya Nne ya Viwanda” yenye kusifika kwa sababu ya uwepo wa teknolojia za kidijitali.

Mataifa mengi duniani kwa sasa yanajulikana kuwa ni mataifa ya kidijitali, kwa sababu ya kutumia teknolojia hii.

Lakini je, taifa la kidijitali lina sifa gani hasa? Jibu hili kwa muktadha wa Tanzania linaweza kujibiwa kwa kutumia maudhui ya Mkakati wa Taifa wa Intaneti yenye Kasi; Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali; na Mwongozo wa Mageuzi ya Kidijitali.

Kwa mujibu wa nyaraka hizi, Dira ya Tanzania kuhusu Taifa la Kidijitali ni kuwa taifa linalobuni, kusimika na kutumia teknolojia ya kidijitali kama nyenzo ya kukuza nguvu za kiuchumi, kuimarisha ustawi wa jamii, na kutegemeza utawala bora.

Teknolojia ya kidijitali ni teknolojia ya habari na mawasiliano, inayojumuisha kompyuta, simu, na program zinazoweza kurahisha utendaji wa kazi kulingana na mahitaji ya kissekta.

Katika fasili hii, kuna mambo matatu; uchumi wa kidijitali, jamii ya kidijitali na dola ya kidijitali. Neno “dola” linarejea vyombo vikuu vitatu vya dola, yaani Serikali, Mahakama na Bunge. Kwa hiyo, kuna nguzo kuu tatu za Taifa la kidijitali

linaloitwa Tanzania.

Uchumi wa kidijitali; uchumi wa kidijitali ni uchumi unaotumia teknolojia za kidijitali kuleta kasi, ufanisi na ubunifu katika kilimo, viwanda, fedga, usafirishaji, nishati, utalii na sekta baki za kiuchumi.

Kwa ufupi, uchumi wa kidijitali ni soko la kidijitali, kwa maana ya jumuiya ya wauzaji na wanunuzi wa bidhaa na huduma, ambapo miamala ya mauziano unafanikishwa na tehamu.

Jamii ya kidijitali; jamii ya kidijitali ni jamii ambayo inazo taasisi za kijamii zinazotekeleza majukumu yake kwa msaada wa Tehama. Taasisi hizo ni pamoja na elimu, afya, familia, jumuiya za kidini, na azaki baki.

Dola ya kidijitali; Dola ya kidijitali ni dola ambayo serikali, bunge na mahakama zinatekeleza majukumu yake kwa umma kwa msaada wa tehamu.

Dola ya kidijitali inasimamia mchakato wa kuleta mapinduzi ya kidijitali kwenye sekta ya uchumi na sekta ya jamii. Hiyo, nguzo ya tatu ya Taifa la kidijitali ni kiunganishi za nguzo baki mbili.

Kwa ufupi, taifa la kidijitali linahitaji Tehama, watu wenye ujuzi wa kutumia wa tehamu, na watu wenye utayari wa kifikra wa kutumia teknolojia kujiendeleza na kupata huduma.

Kidunia, Singapore ndiye anatambulika kuwa kiranja mkuu wa mataifa ya kidijitali.

Twende huko tukajifunze.

MABADILIKO YA JA

UONGOZI wa Gazeti la Pambazuko, tunapenda kuchukua fursa hii adhimu, kwa upekee kabisa kukushukuru wewe mpenzi msomaji wetu kwa kuendelea kutuamini na hata kuwa nasi hadi sasa wakati tumefika miezi mitatu tangu kuanza kukuletea gazeti hili kila wiki – bila kukosa.

Katika kipindi chote hicho, kanzidata ya Pambazuko imeendelea kuwa na idadi kubwa ya wasomaji wake, siyo walioko Tanzania tu, ama maeneo mengine ya Afrika, bali hata Ulaya na Marekani ambako tuna maelfu ya wasomaji wetu.

Tangu kuanza kwa gazeti hili, tumekuwa tukipokea mapendekezo ya kutoka kwa baadhi ya wasomaji wetu wakiomba tuanze kuza Pambazuko hata kwa bei ndogo. Tunashukuru sana mawazo na matamano yenu, lakini sisi tunaamini kupata habari ni haki ya binadamu – kama ilivyo chakula cha mwili – kisivyokuwa na ubaguzi, ndivyo hata chakula cha ubongo kisibague, labda walaji wenyewe.

Hivyo, Pambazuko litandelea kumfikia kila mtu BURE. Na kuhimiza naye agawe na kuhimiza wengine kujisajili.

Hata hivyo, kuanzia toleo lijalo, Pambazuko itaanza kupokea matangazo kutoka kwa watangazaji. Katika matangazo, hapa tutakuwa na ubaguzi, hatutapokea matangazo ya wauza bangi na wenye kufanana nao.

Sambamba na hilo, sura ya Pambazuko itabadilika kidogo ikiwamo kuongezwa kwa kurasa ambazo zitabeba habari, makala, uchambuzi na maoni mengi zaidi, kuboresha zaidi maudhui pamoja na kuimarishwa kwa bodi ya uhariri na watendaji wengine.

Tunaomba ushirikiano wenu katika kuhakikisha heri hii ya kupata habari BURE iendelee kwa kuendelea kutusoma na kuhimiza wengine wajiunge nasi.

Simon Martha Mkina
Mhariri Mkuu

Zaeca wamuelewa Rais Mwinyi

Na Jabir Idrissa

MAMLAKA ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) “imemuelewa haraka” Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wa makosa ya ufisadi.

Mamlaka hiyo imeeleza Pambazuko kwamba imefungua kesi tano za makosa yanayogusa “matumizi mabaya ya ofisi ya umma,” “ubadhirifu wa mali na fedha” na “kughushi” zikiwakabili watuhumiwa 13, wote kasoro wawili, wakiwa ni watumishi wa umma.

Mkurugenzi Mkuu wa Zaeca, Ali Abdalla Ali, aliyeteuliwa hivi karibuni baada ya Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Khamis Ahmed Makarani kujuzulu, alisema katika kesi ya kwanza Namba 84/2022, wahusika ni watumishi wawili wa Ofisi ya Mtafwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Watumishi hao ni Issa Ramadhan Senga (56), Ofisa Manunuzi na Fadhil Ali Hassan (48), Ofisa Takwimu ambao wanashtakiwa kwa ubadhirifu wa mali ya umma na mapato kinyume na Kifungu 42(1) (a) (68)(1)(2) (a) na Kifungu 61 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi, Na. 1/2012.

Kesi nyingine Namba 86/2022 inawahusu wahasibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na wamiliki wawili wa kampuni binafsi za ukandarasi.

Hawa ni Issa Barakat Abdalla (42), Mhasibu Msaidizi wa Wizara na Said Shaaban Mintanga (38) ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Skrafu Investment and Engineering Limited na kampuni ya SAS Construction Limited. Mwingine ni Suleiman Hamad Rashid (63) anayemiliki kampuni ya SH Traders and Fumigation.

Wote wanashtakiwa kwa makosa ya



Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi

ubadhirifu wa mali na mapato kinyume na Kifungu 42(2)(a)(iii) na matumizi mabaya ya ofisi kinyume na Kifungu 53 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Pia wakituhumiwa kwa kosa la ubadhirifu wa Sh. 1,335,730,534.

Kesi Namba 85/2022 inawahusu watumishi watano wa Bodi ya Mapato Zanzibar (Zanzibar Revenue Board -ZRB): Kassim Idrisa Mussa (36) Meneja wa Kitengo cha Mapato ZRB; Abdulatif Abdalla Wazir (26) Ofisa Tehama ZRB; Fatma Kombo Mohd (35) Ofisa Kitengo cha Tehama ZRB na Asia Abdisalami Hussein (44) Mkuu wa Kitengo cha Mapato ZRB.

Wanatuhumiwa kutumia vibaya mali kinyume na Kifungu 43; na matumizi mabaya ya Ofisi kinyume na Kifungu 53 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Namb. 1/2012.

Kwa pamoja wanashtakiwa kwa kujipatia Sh. 278,469,668.68 pamoja na Dola za Marekani 103,817.72, baada ya kuuchezea mfumo wa ukusanyaji wa kodi uitwao ZITAS na kutoa risiti ambazo hazikuingia katika hesabu za bodi hiyo.

Kifo kuwa hiari kufikia mwaka 2045

Na Mwandishi WETU

MWAKA 2018, wanasayansi wawili wabobezi – wakiitwa wahandisi wa mwili na vinasaba, walizundua kitabu chao Jijini Barcelona, Hispania ambako walikuja na matokeo ya utafiti wao kwamba binadamu anaweza kuishi milele, ikiwa ataamua.

Wataalamu hao wa uchunguzi wa kisayansi kwenye mwili wa binadamu ni Dkt. José Luis Cordeiro wa Venezuela na Dkt. David Wood kutoka Uingereza, ambao katika kitabu chao kilichopewa jina la ‘Kifo cha Kifo,’ wanaeleza kuwa ifikapo mwaka 2045, kufa itakuwa hiari na asiyependa na kuwa na uwezo, basi anaweza kuishi miaka atakayochagua yeye.

Kwamba matokeo ya uchunguzi wao kamwe hauhusishi vifo vinavyotokana na kujinyonga, kupata ajali au kufia vitani.

Wanachozungumza wanasayansi hao ni vifo vinavyotokana na uzee na siyo sababu zingine.

Wengi waliohudhuria hafla hiyo ya uzinduzi wa uchunguzi wao, walionekana kuwa na shaka kuu, wakieleza kuwepo na shaka kubwa ya usahihi wa matokeo yao, lakini kadri muda unavyosonga, wapo wanaoanza kuamini matokeo ya uchunguzi huo wa kisayansi.

Kwamba katika dunia ya sasa ya ukomavu wa sayansi na tiba; vinasaba, seli na nyama za mwili na viungo vingine, ikiwamo moyo, vinaweza kuimarishwa kupitia ‘misuli’ na kufanya viungo hivyo kudumu kwa muda mrefu.

Wanazuoni hao wanabainisha kuwa ni vyema kuanzia sasa uzee ukaainishwa kuwa ni ugonjwa na kwamba unaweza kudhibitiwa kwa kutumia utalaamu wa kisayansi.

Wakitetea hoja zao za matokeo ya uchunguzi, wanasayansi hao wanasema kuwa mchakato wa kuondoa uzee utahusisha kugeuza jeni ‘mbaya’ kuwa zenye afya, kuondoa seli zilizokufa kutoka kwenye mwili, kurekebisha seli



David akiwa na Jose wakionyesha kitabu chao kilichoandikwa kwa Kihispania (Picha ya mtandaoni)

zilizoharibiwa, matibabu na seli shina.

Wanasema kwamba kuzeeka ni matokeo ya ‘mikia’ ya DNA, inayojulikana kama ‘telomeres’, katika kromosomu - ambayo kila seli isipokuwa ya damu nyekundu ni fupi, na kuondoa uzee kutahusisha kurefusha hizo telomeres.

Telomeres huharibika na kufupishwa kadiri muda unavyopita, mchakato unaoharakhisha katika tukio la sumu kuingia mwilini - uvutaji sigara, pombe na uchafuzi wa hewa ni miongoni mwa vipengele vinavyopunguza urefu wa telomeres, hivyo kuongeza kasi ya kuzeeka.

Cordeiro na Wood wanaamini kuwa ndani ya miaka 10 ijayo kuanzia sasa, magonjwa yanayohusiana na saratani yatatibika kirahisi kutokana na kukua kwa sayansi ya tiba.

Taarifa za hivi karibuni kuhusu maendeleo ya uchunguzi wao zinaeleza kuwa wameanza kuhusisha watu kadhaa wenye umri mkubwa – kuanzia miaka 70 nchini Columbia, ambako hakuna sheria inayoziua uchunguzi wao.

Inaelezwa na wanasayansi hao kuwa kuna matumaini makubwa ya kuidhibirishia dunia kwamba uchunguzi wao hatimaye utahibitika kwa kiwango kikubwa.

•Makala haya yameandikwa kwa msaaada wa mapitio kadhaa ya kitabu hicho.

Sababu za kuogopa uraia pacha

Na Godwin CHILEWA

MJADALA wa kwanini Tanzania inaogopa kuwa na sheria ya uraia wa nchi mbili – maarufu uraia pacha, haujakoma. Umeendelea kwa miaka mingi na haujapata majibu yanayoeleweka.

Hata hivyo, hivi karibuni ilielezwa kuwa serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, iko mbioni kupeleka muswada bungeni ambao baadaye utakuwa sheria kuhusu hatma ya Watanzania walioko nje ya nchi, ambao waliukana Utanzania wao.

Ifahamike kuwa sheria za Tanzania zinakataza wananchi wake kuwa raia wa nchi mbili au zaidi.

Ikiwa sheria hiyo – ikiitwa ‘Sheria ya Hadhi Maalum’ itaanza kutumika, bado inadaiwa kuwa na ukakasi kwani inawanyima Watanzania hao uhalali wa mambo muhimu, ikiwamo umiliki wa ardhi na kupiga kura.

Je, ni nini kinawatia woga serikali kukataa uraia pacha?

Watanzania wengi wanaamini kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasita kuruhusu uraia pacha kwa sababu ya hofu ya kufungua mlango kwa raia wa kigeni kuvamia na kumiliki rasilimali zilizopo, hususan ardhi.

Ileweke kwamba nchi inapotunga sheria inayoruhusu uraia pacha kwa watu wake, haiwezi kuzuia raia wa nchi nyingine nao kuomba uraia wa nchi hiyo (mutual benefits).

Hii ina maana endapo sheria itakayotungwa ikimruhusu Mtanzania kubaki na uraia wake wakati amepewa uraia wa Uingereza (kwa mfano), sheria hiyohiyo itatumika kumruhusu Muingereza kubaki na uraia wake kama akipewa uraia wa Tanzania.

Utaratibu huu unadhaniwa kuwa utavutia wageni wengi wanaotamani kumiliki ardhi na rasilimali za Tanzania ambazo kwa sasa ni haki ya Watanzania tu.

Kenya imeweza kupitisha haraka



Rais Samia Suluhu Hassan

sheria ya uraia pacha kwa sababu nchi hiyo ina historia ya siasa na uchumi wa kibepari na kikabaila, jambo lililofanya ardhi yote igawanywe na kumilikishwa kwa watu binafsi, na vizazi vyao.

Utaratibu huo umesaidia sana kulinda ardhi ya Wakenya isiporwe na wageni bila ruhusa ya mmiliki ambaye ni mtu binafsi (raia wa Kenya).

Pia zipo dalili kuwa serikali ina hofu ya wanadiaspora kujiingiza katika vyama vya siasa na hasa upinzani, jambo linaloweza kukitia chama tawala matatani kwa kuwa wataruhusiwa kupiga kura kuchagua kiongozi wa nchi, hivyo kuathiri “ushindi” wa chama tawala.

Historia imeonesha kuwa watu wengi wanaoishi nje ya nchi hujenga fikra za kimapinduzi, zinazoongozwa na uhuru wa mawazo na haja ya kuwa huru kisiasa na kiuchumi, hivyo tishio kwa uhai wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

•Mwandishi aliwahi kuwa ofisa wa Idara ya Usalama Tanzania kwa muda mrefu kabla ya kuhamia Marekani kwa shughuli zake za kanisa.

Tutakumbuka Daima...



Kwamba Tanganyika na Zanzibar zilikuwa na viongozi mahiri waliokuwa na hiari ya kupotepa maisha kwa ajili ya ukombozi wa nchi zao. Hawa ni baadhi ya viongozi waliokusanya idadi kubwa ya wafuasi kutokana na mapenzi kwa nchi na kutukuka kwa utumishi wao na hata kuhakikisha utawala wa kimabavu wa Sultan huko Zanzibar na Malkia wa Uingereza huko Tanganyika unakoma. Pichani ni Sheikh Thabit Kombo Jecha (kushoto) aliyekuwa mshauri na msaidizi wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar; Abeid Amani Karume, akiwa na Oscar Kambona aliyekuwa mshauri wa Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Nyerere. Kambona ndiye alikuwa waziri pekee aliyezima yaliyo tajwa kuwa ni maasi ya wanajeshi wa Kambi ya Colito (sasa Lugalo) wakati viongozi wote wa serikali wakiwa mafichoni, Januari 19, 1964. Viongozi wote hawa sasa ni marehemu. (Picha kutoka maktaba).

Marais kupanda basi siyo kosa

Na Abbas MWALIMU

KUMEKUWA na mijadala mingi kuhusu baadhi ya viongozi wa Afrika kupakiwa kwenye usafiri wa gari moja (basi) wakati wakielekea kwenye ibada ya mazishi ya kiongozi wa Uingereza, Malkia Elizabeth II aliyefariki dunia Septemba 8, mwaka huu.

Kimsingi, hawakuwa viongozi wa Afrika pekee waliopanda kwenye mabasi, bali viongozi wengi walioalikwa walitumia usafiri huo unaoweka abiria wengi pamoja.

Baadhi ya marais waliopanda kwenye basi kutoka Afrika ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan wa Tanzania, Rais William Ruto wa Kenya, Paul Kagame wa Rwanda, Tukumbuke kuwa tukio lile lilikutanisha viongozi wakuu wa nchi na serikali, wawakilishi zaidi ya 500 kutoka nchi na taasisi mbalimbali duniani, hivyo maandalizi ya usafiri yalihitaji kuratibiwa vizuri.

Baadhi ya viongozi waliopanda mabasi ni Waziri Mkuu wa Ireland, Micheál Martin, Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, Waziri Mkuu wa Australia, Anthony Albanese, Waziri Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern, Mfalme Abdullah II wa Jordan na mkewe, Malkia Rania.

Aidha, wengine waliopanda mabasi ni Rais wa Malaysia Agong Al-Mustafa Billah Shah, Rais wa Singapore Halimah Jacob, Mfalme wa Japan Naruhito, Rais wa Poland Andrzej Duda, na Rais wa Ujerumani Frank-Walter Steinmeier.

Vilevile walikuwamo wafalme na malkia kutoka nchi zenye mfumo huo wa uongozi.

Matukio makubwa kama mikutano au msiba kama ule wa Malkia Elizabeth II ambao ulikutanisha viongozi wengi njia rahisi ya kuwafikisha katika tukio kwa muda uliopangwa ni kutumia usafiri wa pamoja.

Tufahamu kuwa matukio ya namna ile yanaongozwa na itifaki (protocol) na



Basi lililobeba baadhi ya viongozi wa Afrika kwenye kushuhudia maziko ya Malkia Elizabeth II Septemba 19, 2022.

miongoni mwa mambo muhimu katika protocol ni muda.

Sasa tujiulize kama kila kiongozi angepangiwa muda wake na msafara wake (motorcade) hali ya msongamano ingekuwaje?

Ni muda gani ungetumika kukamilisha idadi ya viongozi wote kufika Westminster Abbey, mahali ambako Malkia alikuwa akizikwa?

Ifahamike kuwa katika matukio kama lile na yafananayo nalo, utaratibu wa usafiri na malazi huratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya nchi husika.

Katika muktadha huu, suala la usafiri wa viongozi wa nchi na serikali liliratibiwa na Ofisi ya Masuala ya Kigeni, Jumua ya Madola na Maendeleo (FCDO) ya Uingereza.

Utaratibu huu hufanyika ili kurahisisha usalama wa viongozi mbalimbali duniani kwa wakati mmoja na hii ni kwa sababu itifaki na usalama wa viongozi ni mambo yanayoenda pamoja na kamwe hayawezi kutenganishwa.

Ileweke kuwa hii siyo mara ya kwanza kwa viongozi kupakiwa kwenye mabasi kwa sababu hata katika Mkutano wa Jumua ya Madola mwaka 2018 (CHOGM2018) uliofanyika London na Windsor, Uingereza, viongozi kutoka nchi zaidi ya 54 walipakiwa kwenye mabasi kwenda na kurudi kwenye mikutano kwa siku zote.



Ukanushi katika Kiswahili

Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Ukanushi katika Kiswahili ((**Negation in Kiswahili**)) unajitokeza katika

hudondoshwa na silabi ya mwisho ya kitenzi huwa -i isipokuwa kwa vitenzi vyenye asili ya Kiarabu. Katika wingi kiambishi cha nafsi hakidondoshwi. (Prefixes for negation in Kiswahili differ according to personal pronoun. Also, tense and personal pronoun prefixes are dropped and the final vowel of the verb changes to -i, except for verbs from Arabic. In plural, the personal pronoun prefix is not dropped.)

Examples			
1 st Person	Singular	Affirmative	Ninacheza mpira (I'm playing football)
		Negative	Sichezi mpira (I'm not playing football)
	Plural	Affirmative	Tunapika wali (We are cooking rice)
		Negative	Hatupiki wali (We are not cooking rice)
2 nd Person	Singular	Affirmative	Wewe unakimbia (You are running)
		Negative	Wewe hukimbii (You are not running)
	Plural	Affirmative	Nyinyi mnacheka (You are laughing)
		Negative	Nyinyi hamcheki (You are not laughing)
3 rd Person	Singular	Affirmative	Yeye analia (He/she is crying)
		Negative	Yeye halii (He/she is not crying)
	Plural	Affirmative	Wao wanaondoka (They are leaving)
		Negative	Wao hawaondoki (They are not leaving)

nje zote na katika hali timilifu na mazoea. Leo tutajifunza jinsi ukanushi unavyojitokeza katika njeo iliyopo. Pia, tutazingatia nafsi. (Negation in Kiswahili features in all tenses and in perfect and habitual aspects. Today we will learn how negation occurs in present tense. We will also consider personal pronouns.)

Ukanushi katika Njeo Iliyopo (Negation in Present Tense)

Viambishi vya ukanushi katika njeo iliyopo hutofautiana kulingana na nafsi. Pia, kiambishi cha njeo na nafsi

Mifano inaonyesha kuwa nafsi ya kwanza wingi, ya pili wingi na ya tatu umoja na wingi hutumia ha- ilhali nafsi ya kwanza umoja ni si- na nafsi ya pili umoja ni hu-. Vyote hutokea mwanzoni mwa neno (Examples show that, the 1st plural, 2nd plural and 3rd singular/plural take ha- while 1st singular is si- and 2nd plural is hu-).

•Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Montini: Sheria ya ndoa na uzazi - 3

Na Deusdedith KAHANGWA

Katika hoja ya saba, tunaweza kusema kwamba, ndoa ni “muungano” kati ya watu wawili wa jinsi tofauti waliokubaliana kuishi pamoja wakiwa mke na mume.

Upekee wa muungano wao ukitokana na tendo la ngono ya jenitalia kwa jenitalia ambalo linaweza kuwa sababu, na hivyo kuwa alama, ya matokeo matano yafuatayo: umoja, uzazi, utulivu, uaminifu, na udumifu kwa muda Fulani.

Hii tutiite “kanuni ya utano wa maisha ya ndoa.” Lakini, neno “muungano” lililotajwa hapo juu, ni dhana ya kifalsafa inayohitaji ufafanuzi kidogo.

Muungano wa kitu ni hali ya kitu hicho kutokuwa na mgawanyiko kwenye sehemu zake za ndani, isipokuwa mgawanyiko mmoja ulio katika mpaka unaokitenganisha kitu hicho na vitu baki vilivyo katika mazingira yake.

Hii maana yake ni kwamba, vitu viwili vitakuwa na “muungano” endapo tu kuna kitu cha tatu kinachoviunganisha na kuvifanya viunde kitu kimoja kikubwa zaidi. Kwa mfano, kuna umoja kati ya matairi manne ya gari kwa sababu matairi hayo ni sehemu ya gari moja linalosafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Kwa ujumla, kutokana na aina ya kitu kinacholeta “umoja” kati ya vitu viwili, tunaweza kupata aina tofauti za umoja.

Kuna muungano wa vitu vilivyokalia kipande kimoja cha kijiografia na kuna muungano wa vitu vilivyokalia kipande kimoja cha majira.

Kuna muungano wa vitu vinavyoshirikiana katika kutekeleza mradi mmoja, yaani “praxiological union.” Kuna muungano kati ya sababu na matokeo, yaani “etiological union.”

Kuna muungano kati ya vitu vinavyofanya kazi sambamba, lakini kwa ajili ya kufanikisha lengo moja



Montini

pana, yaani “teleological union.” Kuna muungano kati ya kitu kizima na sehemu zake, yaani “mereological union.” Na orodha inaendelea.

Kwa mfano, ni muungano kati ya viungo vya mwili kama vile moyo, mapafu, ini, figo, na tumbo la chakula, ambavyo vinao muungano wenye sifa zote hizi. Lengo lake ni kudumisha maisha ya mwili mmoja wa binadamu.

Kwa mujibu wa Montini, “muungano kati ya watu wawili wanaofanya tendo la ngono ya jenitalia kwa jenitalia linaloweza kusababisha mimba,” ni “muungano unaoweza kusababisha uzazi,” endapo vigezo vyote vya kibayolojia vitatimia.

Na hoja ya nane, ambayo ni ya mwisho katika mfululizo wa makala haya, ni hoja kuhusu “mafungamano kadhaa yanayotokana na fasili ya ndoa” Hoja hii inao muundo ufuatao:

Kwamba, kuna uhusiano usiotenganishika kati ya kitu kizima na sehemu zake; kwamba, maana ya umoja, uzazi, utulivu, uaminifu na udumifu ni

Montini: Sheria ya ndoa na uzazi - 3

Inatoka Uk. 17

sehemu tano za kitu kimoja kinachoitwa ndoa; na kwamba, kwa hiyo, kuna uhusiano usiotenganishika kati ya sifa tano zinazotambulisha ndoa;

Kwamba, kumega kigezo chochote kutoka kwenye seti kuu ya vigezo vitano vinavyotambulisha ndoa ni kubadilisha maana ya ndoa. Na kwamba, kwa hiyo, kila moja ya seti ndogo 31 zinazotokana na seti kuu ya vigezo vitano vinavyotambulisha ndoa, ni seti ya sifa za lazima kwa ajili ya kutambulisha ndoa.

Seti ndogo hizo ni pamoja na seti ya “maana ya uzazi na maana ya umoja,” seti ya “maana ya utulivu na maana ya uaminifu,” na orodha inaendelea. Kila seti inatusaidia kusisitiza jambo fulani kuhusu umuhimu na upekee wa ndoa.

Katika kitabu chake, Montini alichagua kusisitiza uhusiano usiotenganishika kati ya “maana ya uzazi na maana ya umoja.” Hii ni kauli aliyoikusudia isisitize vigezo vya kutofautisha ndoa zinazotumia kingamimba dhidi ya ndoa zizozotumia kingamimba. Huo ndio ubunifu wa kipekee utakaomfanya Montini akumbukwe milele kwenye ulimwengu wa wanafalsafa.

Lakini, mawazo ya Montini yanatuwezesha kusema jambo ambalo yeye hakusema. Ukweli ni kwamba, seti ya matendo ya ngono yanayofanywa na mke na mume inaweza na inapaswa kujumuisha matendo ya aina mbili. Kwanza, kuna matendo yenye maana ya umoja na maana ya uzazi kwa mpigo. Na pili, kuna matendo ya ngono yenye maana ya umoja, lakini hayana maana ya uzazi.

Kwa mfano tendo la ngono inayoambatana na kingamimba ya mpito ina maana ya umoja, lakini haina maana ya uzazi. Ni sawa na leo kutumia neno “mbuzi” kumaanisha “mnyama anayefugwa.” Na kesho ukalitumia



kumaanisha “kifaa cha kukuna nazi.”

Maana zote mbili hazifutiki kwenye kamusi. Hivyo, kuna tofauti kati ya kusitisha maana ya alama na kufuta maana ya alama. Montini akifufuka leo na kusoma makala haya atakubaliana nami.

Kwa kuwa ndoa ni taasisi kwa ajili ya kumuunganisha mwanamke na mwanamume, ambao sasa wanaweza kuwa baba na mama wa watoto wao tarajiwa wanapaswa kuweka umoja wao katika misingi ya kuheshimiana.

Kwa kuwa sheria za nchi zinapositiza umoja, uzazi, uaminifu, utulivu na udumifu wa ndoa, sekta ya kiraia inanufaika zaidi na serikali inatua mzigo wa baadhi ya majukumu;

Kwa kuwa, matumaini ya taifa yako mikononi mwa raia wenyewe wanaoelewa ndoa ni kitu gani na pengine hata wale wanaoamini kuwa siyo kitu cha maana, lakini umuhimu wa ndoa unabaki palepale.

Ni kutokana na kuwepo mitazamo hiyo kiznani, na kwa kuwa sheria za Bunge ni “mwalimu” wa jamii; hivyo basi, sheria yetu ya ndoa ifanyiwe marekebisho ili iwe “mwalimu” bora zaidi kuliko hali ilivyo leo.

Serena astaafu tenisi, aenda kuongeza familia

Na Shabaan LULELA

Serena Williams, mmoja wa wanamichezo bora waliowahi kutokea duniani, ameamua kustaafu mchezo wa tenisi na kwamba sasa anageukia “kuongeza” familia na kusimamia vyema biashara zake.

Bingwa huyo wa tenisi mara 23 kupitia Grand Slam kwa mchezaji mmoja mmoja – akiwa raia wa Marekani, amesema amelazimika kuchukua uamuzi huo, siyo kwa kushuka kwa kiwango chake, la hasha! Bali anapumzika na kupata muda mzuri wa kufanya mambo mengine.

Akizungumza kupitia jarida maarufu linaloandika “watu wenye majina makubwa duniani,” la Marekani - Vogue, Serena (40) anasema hapendi neno “kustaafu,” na kwamba anapenda watu watumie neno “mageuzi” zaidi, kwani siyo kwamba anakwenda kujitenga na mchezo anaoupenda sana.

“Sijawahi kupenda neno kustaafu,” labda neno bora zaidi la kuelezea kile ninachokusudia ni mageuzi. Ni kwamba ninabadilika kutoka kucheza tenisi, kuelekea vitu vingine ambavyo ni muhimu zaidi kwangu kwa sasa,” anaongeza mwanadada huyo mwenye binti mmoja, Alexis (5).

Serena alianza kushiriki mashindano makubwa ya tenisi akiwa na miaka 14, mwaka 1995 hadi sasa anapoamua kustaafu. Akiwa na umri wa miaka 17, alishinda mashinano makubwa ya mchezo huyo yanayoitwa US Open (nehini Marekani).

Katika kipindi cha miaka 26, ameshikilia nafasi ya kwanza kwa viwango vya juu vya mchezo huo duniani, kwa upande wa wanawake. Amekuwa namba moja kwa wiki 319.

Katika kipindi cha uchezaji wake,



Serena Williams

inakadiriwa kuwa amekusanya kiasi cha fedha kinachoelezwa kufikia dola za Marekani milioni 100 (sawa na Tsh. Biloni 230) ikiwa ni zawadi kwa ushindi wa vikombe kadhaa. Bado ana fedha nyingi anazopata na anaendelea kupata kupitia matangazo ya bidhaa na hata huduma, kutoka kampuni nyingi za Marekani.

Imeandikwa kwa msaada ya gazeti la The Guardian la Uingereza.

PICHA KUBWA



Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa, akifurahia kununua tikitimaji kutoka kwa muuzaji wa Soko la Mbuyuni, Moshi – Septemba 15, mwaka huu wakati akiwa katika ziara ya kutambua maeneo ya nchi baada ya kuwasili nchini humo. Kawaida katika soko hilo, tikitimaji la ukubwa huo huuzwa kati ya Sh. 5,000 hadi 6,000, lakini furaha ya balozi huenda alipata punguzo! (Picha kutoka Twitter ya balozi huyo).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (TAMPA). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

